

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA SEDP II

Halmashauri ya Wilayaya Misungwi ni moja kati ya Halmashauri zinazitekeleza miradi ya SEDP II awamu ya pili. Katika mwaka 2015/2016 Halmashauri ilipokea jumla ya Tshs 367,737,782.00 ikiwa ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika shule 3 za sekondari ambazo ni Nyabumhanda, Shilalo na Ilujamate. Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na vyumba vinne vya madarasa na matundu manane ya vyoo(Nyabumhanda sekondari), nyumba ya walimu six in one, matundu manane ya vyoo vya wanafunzi na matundu mawili ya vyoo vya walimu(Ilujamate Sekondari) na, ukarabati wa vyumba 2 vya madarasa na ujenzi wa matundu mawili ya vyoo vya walimu(Shilalo Sekondari)

HALI HALISI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI HII KUFIKIA NOVEMBA 30.11.2016.

1. NYABUMHANDA SEKONDARI

Katika shule hii, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:-

- i)* Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa na Ujenzi wa matundu 8 ya vyoo vya wanafunzi jumla ya **Tshs 123,836,935.00** zilitengwa na kutolewa. Jumla ya **Tshs 122,629,300** zimetumika kumlipa mkandarasi. Mradi umekamilika..

Picha chini: inaonyesha majengo la vyumba vinne vya madarasa vilivyokamilika Nyabumhanda Sekondari.





Picha juu: inaonyesha jengo la choo cha wanafunzi chenye matundu manane kilichojengwa katika Shule ya Sekondari Nyabumhanda.



Picha chini: Jengo la choo cha wanafunzi chenye matundu manane likionekana kwa upande wa nyuma.

2. SHILALO SEKONDARI

Katika shule hii, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:-

- i) Shughuli zilizotekelezwa katika Shule hii ni pamoja na ukarabati wa vyumba 2 vya madarasa na ujenzi wa matundu 2 ya vyoo vya walimu. Jumla ya **Tshs 38,502,100.00** zilitengwa na kutolewa. Hadi sasa jumla ya **Tshs 36,064,000.00** zimetumika kumlipa mkandarasi. Mradi umekamilika.



Jengo la kwanza kushoto linaonyesha vyumba viwili vya madarasa vilivyokarabatiwa na kukamilika katika Shule ya Sekondari Shilalo.



Picha ikionyesha jengo la choo cha Walimu Sekondari ya Shilalo kilichokamilika.

3. ILUJAMATE SEKONDARI

Shughuli zilizotekelezwa katika Shule hii ni pamoja na ujenzi wa nyumba moja ya walimu (six in one), matundu mawili ya vyoo vya walimu na matundu manane ya vyoo vya wanafunzi. Jumla ya **Tshs 205,398,747** zilitengwa na kutolewa. Hadi sasa jumla ya **Tshs 190,932,150.00** zimetumika kumlipa mkandarasi.

Picha chini: Jengo la nyumba ya walimu (six in one) Ilujamate Sekondari lililokamilika likionekana kwa upande mmoja wa nyuma.





Picha juu ikionyesha eneo la jiko katika nyumba ya walimu .



Picha juu ikionyesha jengo la nyumba ya walimu (six in one) kwa upande wa mbele wakati mafundi wakiendelea kukamilisha uwekaji wa vioo(alminium)



Jengo la choo cha walimu kilichokamilika katika Shule ya Sekondari Ilujamate.



Picha juu ikionyesha jengo la choo cha wanafunzi wa kike na wa kiume chenye matundu manane kilichojengwa Ilujamate Sekondari.

Nawasilisha.

**Eliurd Mwaiteleke,
Mkurugenzi Mtendaji(W),
MISUNGWI.**